# MWITO WA KUCHUKUA HATUA

## Kutoka Kwa Wavuvi Wadagowadogo*



Wavuvi kwenye ufuo wa bahari Ghana. © Samuel Aboh

Lengo la maendeleo endelevu (SDG) 14.b linatoa mwito kwa nchi **kuhakikisha kwamba wavuvi wadogowadogo wanauwezo wa kufikia rasilimali za bahari na masoko.**

**Tendo** la dharura lahitajika kuangazia changamoto muhimu zifuatazo kuhakikisha ya kwamba uvuvi mdogomdogo umerejeshwa na kulindwa na kuendelea kuchangia uchumi, afya, utamaduni na ustawi.

Wanawake na wanaume wa uvuvi mdogomdogo wa baharini na bara huchangia pakubwa kwa kuchuma riziki, ajira, usalama wa chakula na mapato, kinyume na kubaguliwa na kutengwa kwao katika kufanya maamuzi. Watumiaji wengi wa bahari hutoka kwa jamii ya uvuvi pwani. Kuhakikisha ya kwamba jamii ya uvuvi imenyumbuka na yenye afya bora, wavuvi wadogowadogo wanahitaji njia za upendeleo na madhubuti kufikia kwa bahari iliyonawiri kwa afya bora na mfumo wa ikolojia ili kuteleleza kwa ufanisi majukumu yao muhimu kama walezi na wangalizi wa bahari.

Wavuvi wadogowadogo wanataka serikali ziangazie ukosefu wa msingi wa sayansi, uwazi, usimamizi shirikishi wa uvuvi na tishio la uchavu, ushindani wa maeneo na rasilimali nyingine za viwanda vya uchumi samawati na kuwekeza kwa usimamazi wa mda mrefu wa rasilimali, urejesho wa mifumo ya kiikolojia na ubunifu unaoanzishwa na wanawake na wanaume kutoka kwa jamii ya uvuvi.

## *Serikali sharti...*

### Kwa dharura zihakikishe asili mia moja (100%) ya maeneo ya pwani yana utaratibu wa kudumu wakufikia wenye upendeleo na usimamizi shirikishi

Haki miliki na uwezo wa kufikia rasilimali za uvuvi kwa wavuvi wadogowadogo sharti zilindwe. Wanawake na wanaume wa uvuvi mdogomdogo, lazima washiriki kwa ufanisi katika maamuzi yanayowaathiri.

### Kuhakikisha ushirikishi wa wanawake na kusaidia majukumu yao ya ubunifu

Wanawake wapo katika hatua zote za mnyororo wa thamani wa uvuvi mdogomdogo na ni kiungo muhimu kwa kufikisha samaki kwa watumiaji. Lakini kazi yao haitambuliwi, mchango wao ukijumuisha pia ubunifu, hauthaminiwi na hali yao ya kazi na maisha ni duni.

### Kulinda uvuvi mdogomdogo dhidi ya ushindani wa sekta za uchumi samawati

Athari hasi za sekta zenye nguvu za uchumi samawati za bahari na bara kama vile uzalishaji wa nishati ya bahari, uchimbaji madini kwenye kina cha bahari kuu, utalii, viwanda vya kusaga samaki unga, ukataji magogo ya miti, huhatarisha maisha ya usoni ya jamii za pwani. Mbinu na mtazamo wa tahadhari, uwazi na ushirikishi kamilifu wa uvuvi mdogomdogo sharti utoe mwongozo kwa matumizi yoyote mapya ya bahari.

### Ziwe na uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa uvuvi

Nia na utashi wa kisiasa unahitajika ili kurekebisha kwa dharura sera za uvuvi na utendaji ili kuhakikisha afya bora kwa jamii za uvuvi na manufaa kwa uchumi wa taifa.

### Zijenge jamii thabiti zilizonyumbuka kwa kukabili mabadiliko ya tabia nchi na kutoa matarajio kwa vijana

Wavuvi wadogowadogo ni wa kwanza kudhurika na athari za mabadiliko ya tabia nchi na mishstuko mingine kutoka nje. Hii huathiri maisha ya usoni ya vijana katika jamii. Utawala wa uvuvi sharti ujumuishe uafikiaji wa haki za kijamii na kuhakikisha riziki zinazotegemea uvuvi zenye kwa vijana.



Mvuvi Ureno. © Ivan Gutierrez/SPEA

# *Sasa* ni wakati wa kutenda

*Tunatoa mwito kwa serikali zichukue hatua zifuatazo ifikapo mwaka wa 2030*

## Kwa dharura, zihakikishe asili mia moja (100%) ya maeneo ya pwani yana utaratibu wa kudumu wakufikia wenye upendeleo na usimamizi shirikishi

- Patia wavuvi wadogowadogo haki maalum na za kipekee za uvuvi wa pwani kwa kufunga maeneo ya karibu na ufuo kuzuia uvuvi wa viwandani na vitendo vinginevyo vya viwanda na hali kadhalika, kulinda hati, umiliki, ufikiaji na haki za rasilimali;
- Hakikisha ya kwamba idhini yenye ufahamu na huru imetolewa mbele kwa jambo lolote jipya kwa matumizi ya bahari ikiwemo kwa malengo ya kuhifadhi na maeneo ya hifadhi ya baharini
- Tekeleza mfumo wa usimamizi shirikishi kwa asilimia mia moja (100 %) ya maeneo yote ya pwani kwa kuweka mikakati maalum ya kisheria ambazo zimeweka bayana wajibu na majukumu ya mamlaka na wavuvi, hali kadhalika, kwa kuwezesha wavuvi kushiriki kwa njia ya kufaa (ikiwemo, uangalizi shirikishi na misimu ya uvuvi uliofungwa na kadhalika) na
- Hakikisha fedha tosha katika bajeti ya kila mwaka kusaidia na kuwezesha mifumo hii ya usimamizi shirikishi.

## Kuhakikisha ushirikishi wa wanawake na kusaidia majukumu yao ya ubunifu

- Wezesha wanawake kujratibu kikamilifu na kushirikikiana na mashirika ya kitaalamu na michakato ya maamuzi, pamoja na ile ya maamuzi juu ya usimamizi wa uvuvi.
- Patia uwekezaji kipaumbele katika huduma kama vile kupata maji safi ya kunywa, umeme, mabomba ya maji machafu, vifaa vya kulinda usafi kwenye maeneo ya utengenezaji; miundomsingi ya kuboresha hali ya maisha ya wanawake na ile ya familia zao kama vile makazi bora na vituo vya ulezi wa mchana karibu na maeneo ya utengenezaji; na katika mafunzo juu ya matumizi ya teknolojia mpya.
- Peana uwezo wa kuafiki ardhi na mikopo ili kuuwezesha ubunifu katika mbinu za utengenezaji na uuzaji (tanuri za FTT au jokovu za kutumia nishati ya jua au sola); wezesha mafunzo juu ya kufikia masoko mapya na kustawisha kilimo cha uvuvi mdogomdogo kujalizia utoaji wa malighafi; na
- Ondoa vizuizi vya biashara vilivyomo vya kitaifa na majimbo, hasa ukomeshaji wa usumbufu wa wanawake katika maeneo ya utengenezaji, masoko, njia za biashara na vizuizi mipakani.

## Kulinda uvuvi mdogomdogo dhidi ya ushindani wa sekta za uchumi samawati

- Matumizi mapya ya bahari ambayo yataleta athari hasi kwa mfimo wa ikolojia na jamii wanaozitegemea kwa ajili ya riziki zao zisiruhusiwe na kutegemezwa; na kuhakikisha kuwa idhini huru, ya awali na habari kamalfu inatumika.
- Tengeneza kwa uwazi wa hali ya juu na kwa ushirikishi wa jamii za pwani zinazoathiriwa, utaratibu wa; (1) tathmini huru ya athari ya jamii na mazingira (2) mashauriano yanayoruhusu ufahamu na ushirikishi timilifu wa jamii za uvuvi zinazoathiriwa (3) uamuzi wa migogoro kati ya watumizii wa nafasi za bahari (4) marekebisho ya malalaniko kimahakama na kiutawala na;
- Dhihirisha mgao wa kutosha katika bajeti za kitaifa kuwezesha utekelezaji wa taratibu za mazingira, ikiwemo utekelezaji wa sheria na mikataba ya kimataifa na kanda kabla ya matumizi mapya ya bahari kuruhusiwa

## Ziwe na uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa uvuvi

- Kwa vile uvuvi mdodomdogo hupuuzwa katika takwimu rasmi, hasa wanawake, boresha ukusanyaji wa data za jinsia nyeti na usambazaji wa habariza sekta, ili mchango wao kwa usalama wa chakula, riziki, matumizi endelevu ya bahari zionekane.
- Kutokana na ukosefu wa habari zilizopo, sekta ya uvuvi wa bara ni hafifu kutambuliwa katika sera za kitaifa za uvuvi. Pana haja ya kuhati vizuri uvuvi wa bara, mchango wake na changamoto zinazoikumba ili itambuliwe na kusaidiwa katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.
- Chapisha kima cha chini cha ari ya uwazi wa uvuvi (FITI), taarifa zote husika, ikiwemo sheria, uidhinishaji wa uvuvi, data juu ya utendakazi na mantiki ya utaratibu wa usimamizi.
- Weka wazi kwa umma habari zote kuhusu bahari nyinginezo, miradi ya viwanda vya pwani, bahari na ardhi, ikiwemo ujumbe wa maandashi ya uidhinishaji, vibali na idhini pamoja na taarifa za miradi ya misaada ya kigeni na aina mpya za ufadhili kwa uhifadhi wa bahari ikiwemo hati samawati ya ukopeshaji na ubadilishaji wa deni kwa asili ya viumbe.

## Zijenge jamii thabiti zilizonyumbuka kwa kukabili mabadiliko ya tabia nchi na kutoa matarajio kwa vijana

- Unda pamoja na jamii za uvuvi sera maalum na mipango kukabiliana kwa wepesi na kupunguza ukali wa mabadiliko ya tabia nchi ikiwemo hatua za kerejesha na kuhakikisha afya bora ya ikolojia ya bahari pamoja na zile za kupunguza hatari za majanga na  mipango ya majibu ya dharura.
- Saidia mipango ya kuboresha unyumbukaji wa jamii, hasa zinazokabiliwa na upungufu wa rasilimali, kuwasaidia kupunguza hasara ya mavuno baada ya kuvunwa au kuunda usambazaji mbadala kwa malengo  ya kuwapa vijana matazimio ya riziki za mda mrefu zenye heshima.
- Hakikisha nafasi ya uwakilishi wa kidemokrasia wa halali na ufanisi kwa wavuvi wadogowadogo.
- Hakikisha haki za kijamii kwa wavvuvi wadogowadogo kama vile kupata usalama wa jamii, afya, elimu, usalama baharini utaboresha uvutio wa sekta hii kwa vijana.


Mchakataji Samaki Mwanamke Indonesia. © KNTI.

# *Tunatoa mwito kwa serikali...*

...na wabia wao wajenge jamii za wavuvi wadogowadogo walionyumbuka kwa kuandaa mipango mikakati ya kitaifa kutekeleza vitendo hivi kufikia mwaka **wa 2030**.



Mvuvi Mwanamke Fiji. © Shiri Ram/WCS.

Mipango hii **lazima ifadhiliwe maridhawa** na kuelekezwa na miongozo ya FAO ya kudhibiti uvuvi mdogomdogo endelevu na sera nyenginezo za kanda.**

Tutakuwa tukifuatilia maendeleo na utekelezaji wa mipango hii ya utendaji na tutatoa mwito wa usaidizi kutoka kwa mashirika washiriki na asasi za kiraia kusaidia sisi kufuatilia maendeleo.

www.cffacape.org/ssf-call-to-action

## *Waekaji Saini*

Waekaji saini wote ni mashirika yanayowakilisha vyama vya uvuvi mdogomdogo duniani, ikiwemo Afrika (CAOPA), Pacific (LMMA), Caribbea, kusini (CONAPACH), Amerika ya kati (RAMPR), na Uropa (LIFE Aktea). Tembelea tovuti ili uone waekaji saini wote pamoja na asasi za kiria nyingine na mashirika yasio ya kiserikali yanayosaidia mwito huu.

Unga Mkono

International Year of Artisanal Fisheries and Aquaculture 2022

**VIDOKEZO**

*Kulingana na Miongozo ya hiari kwa ajili ya kuhakikisha uvuvi mdogomdogo ulio endelevu kwa muktada wa usalama wa chakula na kuondoa umaskini (FAO VGSSF), uvuvi mdogomdogo una jumuisha vitendo vyote ndani ya mnyororo wa thamani – kabla ya mavuno, mavuno na baada ya mavuno.

**Miongozo ya hiari kwa ajili ya kuhakikisha uvuvi mdogomdogo ulio endelevu kwa muktada wa usalama wa chakula na kuondoa umaskini" (VGSFF) uliidhinishwa kama chombo cha kimataifa mwezi Juni 2014. Miongozo huu uli buniwa kutokana na historia ndefu ya mapambano ya wavuvi wadogowadogo duniani wakikata rufaa ya kutaka haki zao na jukumu lao katika sekta ya uvuvi nchini mwao zitambuliwe zaidi. // Sera za kanda: Mfumo wa Sera na Mkakati wa Marekebisho ya uvuvi na ufugaji samaki Afrika (AUC-NEPAD 2014.). Sera ya Uvuvi Jumuiya ya Jamii ya Caribbea (CRFM 2020). Mkakati wa Noumea-wimbo mpya za njia ya kubadili uvuvi wa pwani (SPC 2015) na mfumo wa kuinua usimamizi wa uvuvi unao simamiwa na jamii (SPC 2021) wa eneo la Pacific.